BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA UCHUMI KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAAGIZO YA KAMATI KWA WIZARA YA UCHUMI WA BLUU NA UVUVI KWA MWAKA 2021/2022

**Mheshimiwa Spika,**

Nianze hotuba hii kwa kumshukuru Mola Mtukufu kwa kutujaalia neema ya uhai na uzima. Tunaomba Rehema za Mwenyezi Mungu ziendelee kutushukia ili tuweze kutimiza majukumu yetu ya msingi ya kuwatumikia wananchi kwa mujibu wa sheria na kanuni tulizojiwekea.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa moyo mkunjufu kabisa, nakushukuru wewe binafsi Mheshimiwa Spika kwa kunipatia fursa hii adhimu ya kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati ya kudumu ya Uchumi, kuhusu utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Maagizo ya Kamati yetu kwa Wizara ya Uchumi wa Bluu na Uvuvi yaliyotokana na Ripoti ya Kamati kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

**Mheshimiwa Spika,**

Nichukue fursa hii kwa niaba ya Kamati ya Uchumi kumpongeza kwa dhati kabisa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa uongozi wake wa busara uliojaa hekima. Namuomba Mola mtukufu amzidishie afya njema na maisha marefu ili tuzidi kunufaika na uongozi wake.

Aidha, tunatoa pongezi za dhati kwa Makamo wa kwanza wa Rais, Mheshimiwa Othman Masoud Othman kwa msaada mkubwa anaompatia Mheshimiwa Rais katika kutekeleza majukumu ya kila siku ya uongozi wa nchi hii. Vilevile Kamati inatoa pongezi za dhati kwa Makamo wa Pili wa Rais Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla akiwa mkuu wa shughuli za Serikali katika Baraza la Wawakilishi kwa kusimamia vyema majukumu hayo na kuhakikisha ile azma ya Mheshimiwa Rais kuwafikishia wananchi maendeleo inafikiwa.

**Mheshimiwa Spika,**

Ni wajibu wetu kumshukuru Waziri wa Uchumi wa Bluu na Uvuvi Mheshimiwa Suleiman Masoud Makame pamoja na Watendaji wake wote kwa mashirikiano wanayotupatia katika kufanikisha kazi za Kamati yetu. Tunawaomba wazidishe mashirikiano hayo ili kuimarisha utendaji wa shughuli za Kamati katika kuisimamia na kuishauri vyema Wizara hii kwa lengo la kuleta ufanisi.

**Mheshimiwa Spika,**

Pongezi za dhati nazitoa kwa Wajumbe wa Kamati ya Uchumi ambao wamefanya kazi ya ziada katika kufanikisha shughuli za upokeaji wa taarifa za utekelezaji maagizo ya Kamati kwa Wizara zilizo chini ya usimamizi wa Kamati hii. Naomba niwatambulishe Wajumbe wa Baraza lako tukufu Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati kwa majina yao kama ifuatavyo:

1. Mheshimiwa Sabiha Filfil Thani - Mwenyekiti;
2. Mheshimiwa Dkt. Soud Nahoda Hassan - Makamo Mwenyekiti;
3. Mheshimiwa Ameir Abdallah Ameir - Mjumbe;
4. Mheshimiwa Rukia Omar Ramadhan - Mjumbe;
5. Mheshimiwa Panya Ali Abdallah - Mjumbe;
6. Mheshimiwa Hassan Hamad Omar - Mjumbe.

**Mheshimiwa Spika ,**

Kamati yetu ya Uchumi inaundwa na sekretariat ya Makatibu wawili ambao kwa kiasi kikubwa wamekua wakitusaidia kwenye utekelezaji wa majukumu yetu ya kamati makatibu hao ni hawa wafuatao;

1. Ndugu Nouman Thabit Nouman - Katibu; na
2. Ndugu Asma Ali Kassim - Katibu.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mujibu wa Kanuni ya 107(3) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Toleo la 2020 ambayo maelekezo yake yanapatikana kwenye Jadweli la Kwanza, Kamati yetu ina jukumu la kuchambua ahadi zote za Wizara zilizo chini yake kama zitakavyokua zikitolewa katika Baraza na Kufuatilia utekelezaji wa ahdi hizo.

Kwa Mnasaba huo, Kamati yetu ya Uchumi ilikutana na Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi, siku ya tarehe 31/09/2022 na kupokea taarifa ya utekelezaji wa maagizo ya kamati kwa Wizara hiyo yaliyotokana na Ripoti ya Kamati kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

**Mheshimiwa Spika,**

Kiujumla, kwa asilimia kubwa Kamati yetu imeridhishwa na utekelezaji wa maagizo yaliyotolewa kwa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi. Hata hivyo, Kamati haikusita kutoa maelekezo yake katika mambo kadhaa kwa lengo la kuimarisha utendaji wa Wizara ili kuwapatia huduma bora wananchi wenzetu. Kwa mantiki hiyo, Kamati yetu ilitoa maagizo 49 kwa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi yaliyoelekezwa katika nyanja tofauti zifuatazo:-

1. Mamlaka ya Kudhibiti na Uchimbaji wa Mafuta ( ZPRA);
2. Kampuni ya Maendeleo ya Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta (ZPDC);
3. Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Mazao ya Baharini;
4. Idara ya Maendeleo ya uvuvi na mazao ya baharini;
5. Kampuni ya Uvuvi (ZAFICO);
6. Afisi ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi (Pemba);
7. Soko la Tumbe - Pemba;
8. Ukulima wa mwani;
9. Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu;
10. Mradi wa Swiofish.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yetu imeridhishwa na hatua zinazochukuliwa na Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi, kupitia Mamlaka ya Kudhibiti Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta Zanzibar (ZPRA) katika jidihada zake za kuliendeleza suala la rasilimali ya mafuta nchini. Kamati yetu inaitaka Wizara kwa kupitia Mamlaka hiyo kutoa elimu kwa wananchi juu ya mfumo mzima unaotumika kwenye shughuli ya utafutaji na uchimbaji wa mafuta, kwani zoezi hili hadi sasa limechukua muda mrefu na wananchi wamekua wakihoji ni lini haswa mafuta yatapatikana hapa Zanzibar, kwani inajulikana wazi kwamba kupatikana kwa rasilimali ya mafuta kutachochea ukuaji wa uchumi na hata kiwango cha umasikini kwa mtu mmoja mmoja kitapungua.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaipongoza Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kupitia mamlaka ya kudhibiti utafutaji na uchimbaji wa mafuta kwenye zoezi wanaloendelea nalo la ulipaji wa fidia kwa walioathirika na zoezi la mtetemo. Licha pongezi hizo Kamati

inaitaka Wizara kuharakisha zoezi la ulipaji wa fidia kwani kadiri zoezi hilo linapochelewa kutekelezwa na thamani ya fedha zilizokadiriwa kwa wakati huo itakua imeshuka sana na itapelekea kuzuka kwa malalamiko kwa wananchi wenzetu walioathirika na mitetemo hiyo. Sambamba na hilo, Kamati yetu imesikitishwa na baadhi ya wananchi wasiokua waaminifu kuwasilisha malalamiko ya kuwa na wao walikua sehemu ya waathirika wa mitetemo, ilhali hawakujitokeza kujisajili kipindi cha kusajili waathirika jambo ambalo linafanya zoezi la ulipaji wa fidia kusuasua kutokana na kila siku kuibuka kwa walalamikaji wapya. Kwa mantiki hiyo, Kamati inaitaka Wizara kulitafutia ufumbuzi jambo hilo na kuwachukulia hatua wale wenye nia ya kulihujumu zoezi la ulipaji wa fidia.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaipongeza Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kupitia Taasisi ya Utafiti na Mazao ya Baharini kwa hatua wanazozichukua katika suala zima la muundo wa kiutumishi hadi sasa. Kamati inaitaka Wizara kuongeza juhudi juu ya ukamilikaji wa muundo wa Taasisi hiyo, kwani bila ya Muundo wa ofisi, taasisi hiyo itakosa dira ya kujiendesha.

**Mheshimiwa Spika,**

Nitakua mchoyo wa Fadhila ikiwa sitaipongeza Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kupitia Taasisi yake ya Utafiti wa Uvuvi na Mazao ya Baharini kwa matumizi ya teknolojia mpya ya uvuvi, ambayo inampa uwezo mvuvi wa kutambua wapi samaki walipo, wingi wa idadi ya samaki kwa eneo husika na aina ya samaki waliopo. Jambo hili ni la kupongezwa sana kwani, litaepusha ule uvuvi wa kimazoea ambao hauna tija. Sambamba na hilo, Kamati inaitaka Taasisi ya Utafiti na Mazao ya Baharini kuongeza Utafiti Zaidi ili kuhakikisha rasilimali ya samaki inaendelea kupatikana na viumbe vya baharini vilivyokua hatarini kutoweka vinaendelea kuhifadhiwa.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu inaipongeza Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa kuwa wasikivu kwa kusikia kilio cha wavuvi juu ya suala la kupatiwa boti za uvuvi za mita 7 na za mita 8 ambazo hazitoshelezi mahitaji yao. Hivyo baada ya zoezi hili la ugawawaji wa boti za mita 7 na za mita 8 kukamilika, wizara imeshaweka milango wazi kwa wavuvi kuwasilisha mahitaji ya boti zinazoendana na matakwa yao ili Wizara iingiye mikataba na watengenezaji.

Aidha, Kamati inaitaka wizara kutoa elimu kwa wavuvi na wananchi kwa ujumla wasijikite tu kwenye shughuli za uvuvi wa baharini tu bali pia wajihusishe na suala la ufugaji wa matango bahari (majongoo ya bahari) kwani wanatumika kwenye shughuli za utengezaji wa dawa na hivyo kuifanya rasilimali hiyo ya Matango bahari (Majongoo bahari) kuwa na Thamani Kubwa kwenye soko la Kimataifa.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati ya Uchumi inaendelea kuihimiza Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kupitia Idara yake Maendeleo ya Uvuvi, kuendelea kutoa elimu kwa wavuvi juu ya maeneo ya hifadhi na inapotokea kwa baadhi ya wavuvi wanapovunja sheria ni wajibu wa Idara au chombo cha usalama kilichowakamata wavuvi hao kuwafikisha mahakamani ili sheria ichukuwe mkondo wake. Kamati haikubaliani hata kidogo na hatua zinazochukuliwa kwa baadhi ya vyombo vya usalama kuwapiga wavuvi na kuwahukumu apoapo ilihali wao sio chombo cha kutoa haki, sambamba na hilo Kamati inawapongeza Wizara kupitia Idara ya maendeleo ya Uvuvi kwa kuanzisha doria shirikishi kwenye maeneo yote ya uhifadhi wa bahari,jambo hili litasaidia zaidi kwenye kuzuia wavuvi wasiokua na nia njema kuepuka kuyasogelea maeneo hayo,kwani mara nyingi waharibifu wa maeneo ya uhifadhi wa bahari hua wanatoka maeneo hayohayo ya karibu.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati pia inaipongeza Wizara ya Uchumi wa Bluu na Uvuvi kupitia Kampuni ya Uvuvi Zanzibar (ZAFICO) kwa jitihada zake inayochukua ili ifike siku moja iweze kujiendesha wenyewe bila ya kupokea ruzuku Serikalini,wakati huohuo Kamati inaipongeza Kampuni ya Uvuvi Zanzibar (ZAFICO) kwa kununua majiko Zaidi ya 60 ya kuchemshia dagaa hali ambayo, Zanzibar itaondokana na yale mazoea ya zamani ya uchemshaji na uanikaji wa dagaa,ambapo usalama wa mlaji haukuwa wa kuaminika, ila kitendo cha kuja kwa majiko haya yatasaidia sana kuinua soko la dagaa ndani ya Zanzibar na nje ya mipaka ya Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu inatoa Pongezi kwa mara nyengine tena kwa serikali ya Mapinduzi Zanzibar inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt.Hussein Ali mwinyi kwa kusikia kilio cha muda mrefu cha wakulima wa zao la Mwani, Pale alipoamua kukijenga kiwanda kikubwa cha kuchakatia mwani kilichopo Chamanangwe kisiwani Pemba,ambapo ujenzi wake unakwenda kwa kasi sana ,jambo ambalo linaleta matumaini makubwa kwa wananchi wetu na pia kuzidi kuwapa Imani wananchi kuwa ukiahidi jambo basi lazima ulitekeleze. Sambamba na hilo Kamati inaipongeza Wizara ya Uchumi wa Bluu na Uvuvi kwa kupandisha bei ya zao la mwani, jambo ambalo limeongeza hamasa kwa wananchi kuzidi kujiingiza kwenye kilimo hicho na kujiongezea kipato,na kuzidi kulipunguza wimbi la umasikini.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaishauri Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kuendelea kuwapa elimu ya usalama wa baharini wavuvi, ikiwemo kuvaa makoti ya kujiokolea (Life Jacket) hii itawasaidia pindi itakapotokea dharura kuweza kujiokoa. Vilevile Kamati

inaitaka wizara kuwalazimisha manahodha na wavuvi pia wanapoelekea kwenye shughuli za uvuvi kuacha namba zao za simu,ili iwe rahisi pindi ikitokea dharura kuweza kuwasiliana.

**Mheshimiwa Spika,**

Baada ya kutoa maoni hayo ya Kamati yetu ambayo kiufupi yametoa taswira nzima ya mambo ambayo Wizara ya Uchumi wa Bluu na Uvuvi imeyatekeleza. Nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili linalowakilisha wananchi wote wa Zanzibar, kutoa maoni na mapendekezo yao kuhusu utekelezaji wa Maagizo yetu ambayo Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi ameuwasilisha mbele yetu.

**Mheshimiwa Spika,**

Nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa utulivu na usikivu wao wakati wote wa uwasilishaji wa Hotuba hii. Kwa niaba ya Kamati ya Uchumi , naomba kuwasilisha.

Ahsante sana,

……………………………

Mheshimiwa Sabiha Filfil Thani,

Mwenyekiti

Kamati ya Uchumi,

Baraza la Wawakilishi,

**Zanzibar.**